

HALI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI TANZANIA: UDHALILISHAJI WA LUGHA YA TAIFA?

YOHANA P. MSANJILA

The aim of this paper is to analyse data that was collected in 2003 and 2004 in order to ascertain the claim made by Kiswahili stakeholders that the status of Kiswahili in secondary schools in Tanzania has dropped. The findings reveal that the number of periods allocated for Kiswahili is fewer than that for English. Secondly, whenever there is a shortage of Kiswahili teachers, any member of the teaching staff or even non-specialists are called upon to fill the gap. Thirdly, we note that Kiswahili teachers have never had the opportunity to attend any Kiswahili seminar since they graduated from colleges. Fourthly, the Ministry of Education and Culture has issued a circular to schools barring the students from speaking Kiswahili at the school compound to enable them to become proficient in the English language. Considering the above findings, this study confirms that the status of Kiswahili in secondary schools in Tanzania has diminished.

1. Utangulizi

Makala haya yametokana na utafiti uliofanywa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (kwa kifupi, TUKI) mwaka 2003 na 2004 kwa njia ya kuendesha semina za walimu wafundishao somo la Kiswahili katika shule za sekondari Tanzania. Semina hizi ziliendeshwa kikanda nchi nzima; zilianza Februari, 2003 na kumalizika mwezi wa Aprili, 2004. Jumla ya walimu 526 walihudhuria semina hizi kwa nchi nzima. Idadi ya walimu waliohudhuria semina kutoka kila kanda imeonyeshwa katika mabano kama ifuatavyo: Kanda ya Kusini, Mtwara (30) na Iringa (64); Kanda ya Kusini Nyanda za Juu, Mbeya (49); Kanda ya Kaskazini, Moshi (61) na Arusha (65); Kanda ya Ziwa, Mwanza (65); Kanda ya Kati, Dodoma (110) na Kanda ya Mashariki Morogoro (82). Muda wa semina kwa kila kanda ulikuwa siku nne za kazi. Muda huu ulizingatia mada za sarufi na fasihi ya Kiswahili zilizopangwa kutolewa katika semina.

Kabla ya semina hizi kufanyika, Mratibu wa semina wa TUKI alituma barua kwa Wakuu wote wa Shule za Sekondari nchini kuwataka walimu wa Kiswahili waainishe matatizo wanayopata katika ufundishaji wa somo la Kiswahili hususani katika mada za sarufi na fasihi ya Kiswahili na kuyatuma TUKI. Ratiba ya semina ilipangwa kwa kuzingatia mada zenye matatizo zilizoainishwa na walimu wenyewe. Ili kupata maoni ya jumla ya walimu kuhusu somo la Kiswahili, walimu walipangiwa muda katika ratiba ya semina wa kujadili hali halisi ya Kiswahili shuleni wakiongozwa na Mwenyekiti na Katibu waliochaguliwa miongoni mwao. Haya maoni na mapendekezo yaliyotolewa na walimu, yaliwasilishwa kwa majadiliano ya

pamoja kati ya walimu wenyewe, wataalamu¹ mbalimbali kutoka: TUKI, Taasisi ya Elimu, Baraza la Mitihani Tanzania, na Ofisi za Ukaguzi za Kanda. Lengo la majadiliano yalikuwa ni kuweka taarifa sawa na kupata maelezo ya ziada au ufafanuzi kutoka kwa wajumbe wa semina. Kwa kutumia mbinu hii ya majadiliano ya pamoja, hoja mbalimbali zilizotolewa na wajumbe wa semina kuhusiana na somo la Kiswahili zilichambuliwa na kutolewa maelezo sahihi siyo tu na wataalamu wa Kiswahili waliokuwepo kwenye semina bali pia na walimu wenyewe wafundishao somo la Kiswahili shuleni.

Malengo ya semina hizi yalikuwa ni manne: Kwanza, kutathimini hali ya somo la Kiswahili shuleni. Pili, kutoa fursa ya majadiliano na ubadilishanaji wa utaalamu katika ufundishaji wa sarufi na fasihi ya Kiswahili baina ya walimu wa sekondari na wataalamu wa Kiswahili kutoka TUKI na Idara ya Kiswahili zote za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Lengo la tatu lilikuwa ni kuainisha matatizo wanayopata walimu katika ufundishaji wa somo la Kiswahili shuleni na kupendekeza njia za utatuzi wa matatizo hayo. Nne, kutoa mapendekezo kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa na vyombo vinavyohusika na ukuzaji wa Kiswahili ili somo la Kiswahili liweze kufundishwa vizuri na kwa usahihi zaidi.

Katika makala haya tunakusudia kuchambua taarifa muhimu zilizopatikana katika semina hizo na kuzichunguza sambamba na muhtasari wa somo la Kiswahili, sera ya lugha na katika maandiko mbalimbali yahusuyo lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika mfumo wa elimu kwa jumla. Uchambuzi wa aina hii una lengo la kutaka kuthibitisha madai kama Kiswahili kinadhaliwa au kinapewa hadhi yake ya kutumika kama lugha ya taifa katika shule za sekondari kwa kuzingatia mfumo wa elimu wa Tanzania na sheria za shule.

Uchambuzi wa makala yetu unaanza kwanza na kuchunguza sera ya lugha ya Tanzania ili kuona nafasi na dhima ya lugha ya taifa (Kiswahili) na Kiingereza. Lengo la uchunguzi huu ni kuwapatia wasomaji wetu usuli wa kuzielewa lugha zitumikazo katika mfumo wa elimu Tanzania ili waweze kufuata mjadala wa makala haya kikamilifu. Pili, baada ya kuona sera ya lugha ilivyo, tumechunguza mambo yafuatayo: utoshelevu wa Muhtasari wa Kiswahili (Wizara ya Elimu na Utamaduni 1996) utumikao shuleni, utoshelevu wa walimu wa Kiswahili shuleni na mwisho tumechunguza mchango wa Wizara ya Elimu na Utamaduni katika kusi-mamia somo la Kiswahili shuleni. Tatu, baada ya kuona hali halisi ya Kiswahili shuleni, tumetoa mapendekezo yanayolenga kuboresha hali ya Kiswahili katika shule za sekondari. Na tano, tumetoa hitimisho la utafiti wetu.

2. Sera ya Lugha Tanzania

Sera ya lugha ni mwongozo wa kiutekelezaji unaohakikisha kwamba lugha zilizomo katika nchi husika zinatumika sawasawa kulingana na mipango ya nchi hiyo. Sera ya Utamaduni (Wizara ya Elimu na Utamaduni 1997) ya Tanzania ambayo ndani yake imeelezea sera ya lu-

¹ Katika semina hizi za Kiswahili pia walihudhuria wataalamu wengine wa Kiswahili kutoka Taasisi ya Elimu, Baraza la Mitihani Tanzania na Ofisi za Ukaguzi za Kanda. Wataalamu hawa wanahusika na somo la Kiswahili katika kazi zao.

HALI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI TANZANIA

gha, inatambua umuhimu wa kutumia siyo tu lugha ya Kiswahili bali pia lugha za Kigeni (Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani n.k.) na lugha za jamii katika mawasiliano ya kitaifa na kimataifa. Kwa mujibu wa sera ya utamaduni, Kiswahili kimetamkwa kuwa ni lugha ya taifa ya Tanzania. Kinatumika katika shughuli rasmi za serikali, pia kinatumika kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi, vyuo vya ualimu (hususani kwa walimu wa daraja la IIIA), kinafundishwa kama somo la lazima katika shule za sekondari (hususani kidato cha I – IV) na pia ni somo la hiari katika shule za sekondari (kwa kidato cha V na VI) na vyuo vikuu.

Udhaifu wa sera hii ni kwamba haitoi nafasi kwa Kiswahili kutumika katika maeneo muhimu kama vile katika: elimu ya juu, sayansi na teknolojia, Mahakama Kuu na za Rufani, diplomasia na katika biashara za kimataifa. Sera ya lugha imekipa Kiingereza dhima hii ya kutumika katika maeneo haya muhimu siyo kwa sababu Kiswahili hakiwezi bali kikitumika katika maeneo hayo, kwa mawazo yao hadhi ya lugha ya Kiingereza itashuka na kupoteza umarufu wake hapa nchini. Ili kuhakikisha kwamba Kiingereza kinapata nguvu ya kutumika shuleni, sera ya elimu inatamka kwamba Kiingereza kitaendelea kutumika kama lugha ya kufundishia katika sekondari na elimu ya juu na Kiswahili kitaendelea pia kutumika katika shule za msingi. Wakati Sera ya Utamaduni (Wizara ya Elimu na Utamaduni 1997) inatamka kwamba mipango itafanywa ya kukiwezesha Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika ngazi zote za elimu, sera ya elimu inasisitiza matumizi ya Kiingereza na Kiswahili katika ngazi tofauti za elimu. Kupingana huku kwa sera ya utamaduni na sera ya elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili katika elimu ya juu, ndilo tatizo kubwa linalokwamisha maendeleo ya Kiswahili hapa nchini.

Katika kupanga dhima ya kila lugha (k.m. Kiswahili na Kiingereza), sera ya lugha ya Tanzania haikuzingatia hali halisi ya watumiaji wa lugha hizi. Wakati Kiingereza kinazungumzwa na watu chini ya asilimia 10 ya Watanzania wote, kimepewa dhima ya kutumika katika maeneo muhimu kuliko Kiswahili, lugha ya taifa. Kiswahili kinachozungumzwa karibu na Watanzania wote kimeshindwa kupanua matumizi yake katika maeneo haya muhimu mbali na yale yaliyoainishwa katika sera ya utamaduni tu. Tunapenda kutahadharisha hapa kwamba Kiswahili kisipopanua matumizi katika maeneo haya muhimu, mambo ya msingi kama: elimu ya juu, haki za raia, sayansi na teknolojia kwa ujumla yanayotolewa kwa Kiingereza yataendelea kwa muda mrefu kubaki mikononi mwa wateule wachache.

Haitoshi kwa sera ya lugha kutamka kwamba upo mpango maalumu wa kuiwezesha elimu ya juu na mafunzo ya ngazi zote za elimu kutolewa katika lugha ya Kiswahili bila kuweka bayana mikakati ya utekelezaji wa mpango huo. Matamko kama haya katika sera huwekwa kisiasa bila ya kuhusisha wataalamu ambao huhusika na uandaaji wa vitabu vya Kiswahili vitakavyotumika katika ufundishaji. Tunasisitiza kusema hayo ni matamko ya kisiasa kwa sababu hakuna fedha zinazotengwa na serikali kuandaa mabadiliko haya. Kama tulivyosema huko nyuma, sera ya lugha ni mwongozo wa kiutekelezaji unaopaswa kufuatwa siyo tu na serikali bali pia na wadau wote wa Kiswahili kwa ujumla. Sasa, ni kwa kiasi gani somo la Ki-

swahili linafundishwa kikamilifu katika shule za sekondari kwa mujibu wa sera ya utamaduni iliyopo? Sehemu inayofuata inajadili suala hili kwa undani.

3. Hali ya Kiswahili katika Shule za Sekondari Tanzania

Muhtasari wa somo la Kiswahili (1996) unaotumika sasa (2005) katika shule za sekondari Tanzania umeainisha malengo ya kufundisha Kiswahili kama ifuatavyo:

- Kuwawezesha wanafunzi kutumia Kiswahili kwa ufasaha katika fani zote za maisha;
- Kuwawezesha wanafunzi kuelewa kuwa Kiswahili ni sehemu muhimu ya utamaduni wa Tanzania.

Ukichunguza kwa makini malengo haya ya kufundisha Kiswahili utagundua kwamba yanaoana siyo tu na malengo ya elimu bali pia na malengo ya sera ya lugha kwa ujumla. Kusisitiza wanafunzi waweze kutumia Kiswahili kwa ufasaha katika fani zote za maisha na watambue kuwa Kiswahili ni sehemu muhimu ya utamaduni wa Tanzania, maana yake ni kuwataka wanafunzi waitumie lugha ya Kiswahili kikamilifu ili waweze kuwa raia bora kama asemavyo Nyerere (1968: 132) kwamba:

[makusudi ya elimu ni] kuhamisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine mkusanyiko wa busara, hekima na maarifa ya jamii, kutayarisha vijana ili kuwa wanachama wazuri katika jamii na kutoa mchango wao mzuri katika kulinda na kuiendeleza jamii hii.

Vijana wengi wanaomaliza elimu ya sekondari wanategemewa wawe na umilisi wa kuto-sha wa Kiswahili katika kuandika na kuzungumza. Tafiti mbalimbali zilizofanywa hapa nchini zinaonyesha kwamba wanafunzi waliomaliza elimu ya sekondari wana matatizo ya kujieleza siyo tu katika lugha ya Kiingereza bali pia katika Kiswahili (Rubagumya 1996 na 1999; Qorro 1997; Kiputiputi 2001; Msanjila 1988 na 2005).

Zipo sababu mbalimbali zinazosababisha wanafunzi wengi wakose umilisi wa kujieleza vizuri katika maandishi na mazungumzo. Tunaweza kujumuisha pamoja sababu hizi katika makundi makuu matatu yafuatayo: Kwanza ni sababu zitokanazo na muhtasari wa Kiswahili, pili, sababu zinazohusu walimu wafundishao Kiswahili na tatu ni zile sababu zitokanazo na Wizara ya Elimu na Utamaduni. Hebu tuanze kuchunguza sababu ya kwanza.

3.1. Utoshelevu wa Muhtasari wa Kiswahili (1996)

Mada zilizopangwa kufundishwa kwa kidato cha I – IV na kidato cha V – VI kwa mujibu wa muhtasari huu ni hizi zifuatazo: *Lugha, Fasihi Andishi na Fasihi Simulizi, Sarufi, Ufahamu, Utungaji, Utumizi wa Lugha na Historia ya Kiswahili*. Kila mada ina vipengele vyake vidogo kadhaa vinavyopaswa kufundishwa katika kila kidato. Hii ina maana kwamba kila kidato hufundishwa mada hizi saba kwa viwango tofauti kulingana na kidato anachosoma mwanafunzi. Uchambuzi uliofanywa na walimu waliohudhuria semina za Kiswahili za kanda unaonyesha kwamba muhtasari huu una kasoro kuu nne. Kwanza, mada zilizopangwa kufundishwa hazitofautishi bayana viwango vya kidato (Kihore 2001). Pia mada hazizingatii maendeleo ya ta-

HALI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI TANZANIA

aluma na mitazamo mipya ya kinadharia. Vipengele vidogo vinajirudia rudia katika kila mada bila ya kuonyesha tofauti ya uchanganuzi wa kina wa mada kwa kila kidato. Ni rahisi kwa mwalimu asiye na uzoefu wa kutosha wa kufundisha somo la Kiswahili kurudia kufundisha mambo yale yale katika vidato vinavyokaribiana (k.m. kidato cha 1 na 2, kidato cha 3 na 4, na kidato cha 5 na 6).

Pili, mada za fasihi ya Kiswahili hazina vitabu maalumu vya kiada vinavyoelezea nadharia au mikabala mbalimbali ya uhakiki wa vitabu. Katika uhakiki wa vitabu vya fasihi, walimu wameachwa wenyewe wajitafutie maarifa kutoka vitabu mbalimbali. Ingawa utaratibu huu unaonekana ni mzuri bado tunafikiri una kasoro kwa sababu baadhi ya waandishi wa vitabu vya fasihi hawaandiki kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya taaluma bali huandika kwa ajili ya kutafuta fedha. Vitabu vingi vilivyoandikwa kwa namna hii, mambo yake mengi katika fasihi ama huwa yamepotoshwa au yameandikwa kijuu juu bila ya kuzama kwenye taaluma sahihi ya fasihi. Tulichogundua kwenye semina hizo za kanda ni kwamba walimu hawana vitabu vya kuaminika vya fasihi ya Kiswahili vya kuwainua kitaaluma katika masuala ya nadharia na mikabala mbalimbali ya fasihi simulizi na fasihi andishi. Kusoma vitabu mbalimbali vya fasihi bila ya kuwa na msingi imara wa kinadharia, kunaonekana kuwachanganya walimu na wanafunzi pia.

Tatu, idadi ya vipindi 3 vya Kiswahili kwa wiki (kwa ajili ya kidato cha I – IV tu) vilivyopangwa havitoshi kufundisha vipengele vyote vya sarufi na fasihi ya Kiswahili. Walimu wengi waliohudhuria semina za Kiswahili za kanda wanadai kwamba huwa hawamalizi kufundisha mada zote zilizoainishwa kwenye muhtasari kutokana na uchache wa vipindi. Walimu wachache wanaomaliza kufundisha mada zote wanaeleza kuwa baadhi ya mada hasa zile ngumu hufundishwa kijuu juu ili mradi wamalize mada zilizopangwa kwenye mipango yao ya kazi kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi na maafisa wanaohusika.

Inashangaza kuona kwamba Kiingereza kimepangiwa vipindi 6 kwa wiki ikiwa ni mara mbili ya vile vya Kiswahili. Hata kama kigezo kilichotumika kina lengo zuri la kuwapa wanafunzi muda mwingi wa kujifunza lugha ya kigeni wakiwa shuleni, bado kigezo hicho hakiwezi kuwa sababu ya msingi ya kukipunguzia Kiswahili idadi ya vipindi vyake kutoka vipindi 4 vya zamani hadi vipindi 3 vya sasa (2005). Tunapenda ieleweke kwamba zamani vipindi vilipokuwa 4 kwa wiki hakukuwa na mada nyingi za Kiswahili za kufundisha kuliko ilivyo sasa. Hatuoni mantiki kwa nini vipindi vipungue wakati mada za kufundisha zimeongezeka. Maana tunayopata ya kupunguza vipindi vya Kiswahili wakati zipo mada nyingi za kufundisha ni kwamba Kiswahili, lugha ya taifa inashuka hadhi kijamii na kielimu. Kama Kiswahili kingeonekana kuwa kina hadhi na dhima muhimu kitaifa na kimataifa kama ilivyo kwa Kiingereza, basi angalau vipindi vya Kiswahili vingebaki kuwa vile vile 4 vya zamani au kungeongezwa kipindi kimoja zaidi ili viwe 5 kwa wiki badala ya vipindi vitatu (3) vya sasa.

Nne, siyo kawaida kuona kwamba muhtasari hausisitizi matumizi ya kamusi katika kujifunza somo la Kiswahili shuleni. Kamusi ni rejeo muhimu sana siyo tu kwa wanafunzi wana-

ojifunza lugha bali pia kwa walimu wanaofundisha lugha. Akisisitiza umuhimu wa kutumia kamusi, Mdee (2001: 264) anasema:

Maudhui ya kamusi sio maana pekee, bali zipo taarifa nyingine hususani za kisarufi. Tumeona pia kuwa taarifa za kisarufi katika kamusi huweza kumsaidia mwanafunzi kuongeza ujuzi wake wa sarufi ya lugha ambayo ni msingi wa kupata umilisi wa kuiongea na kuandika lugha.

Pamoja na umuhimu huu wa kamusi, walimu wengi waliohudhuria semina za Kiswahili za kanda wanakiri kwamba, siyo tu wanafunzi ambao hawatumii kamusi darasani bali hata walimu wenyewe hawatumii kamusi mara kwa mara. Pale haja ya kutumia kamusi inapotokea, lengo huwa ni kutafuta maana za maneno. Ni walimu wachache sana waliokiri kutumia kamusi mara kwa mara na kikamilifu. Bado ni jambo la kushangaza kuona kwamba walimu wengi hawana kamusi zao wenyewe bali hutegemea kamusi za shule ambazo nazo ni chache sana na hizo chache hufungiwa makabatini ili zisipotee au kuibiwa. Kuna haja ya kuhimiza matumizi ya kamusi na ikiwezekana kila mwanafunzi awe na kamusi yake mwenyewe na utaratibu ufanywe ili kuwe na maswali ya mtihani kwa wanafunzi yanayohusu utumiaji wa kamusi ili kuwajengea wanafunzi umilisi wa lugha ya Kiswahili.

3.2 Utochelevu wa Walimu wa Kiswahili

Kwa mujibu wa mfumo wa elimu Tanzania, walimu wanaokubaliwa kufundisha shule za sekondari ni wale wenye sifa za elimu kuanzia stahhada na shahada ya chuo kikuu. Sifa hizi za elimu ni pamoja na walimu wafundishao somo la Kiswahili. Uchunguzi uliofanywa kupitia semina za walimu wa Kiswahili za kanda unaonyesha kwamba zipo baadhi ya shule za sekondari hasa shule binafsi na zile zilizofunguliwa miaka ya karibuni (miaka 10 iliyopita) zinafundishwa na walimu ambao hawana sifa za elimu zinazotakiwa na Wizara ya Elimu na Utaamaduni. Walimu wa aina hii wapo wa aina tatu: Kwanza, wapo wale walimu ambao huchukuliwa kutoka shule za msingi na ambao huonekana na wakaguzi wa elimu kuwa wana uwezo mzuri wa kufundisha na kwamba matokeo yao ya kidato cha nne ni mazuri. Pili, wapo ambao sio walimu kitaaluma bali ni wahitimu wa kidato cha sita ambao kwa kawaida huwa wapo wakisubiri kujiunga na vyuo vya elimu ya juu. Walimu wa aina hii huajiriwa na shule kwa muda. Tatu, wapo walimu ambao walipokuwa vyuo vya ualimu/chuo kikuu hawakusoma somo la Kiswahili wala hawakujifunza mbinu za kufundisha Kiswahili, lakini kutokana na uhaba wa walimu wa Kiswahili, Wakuu wa shule huwaomba walimu wa masomo mengine kufundisha somo la Kiswahili kwa kutumia maarifa waliyojifunza wao wenyewe walipokuwa wanafunzi wa sekondari.

Tunapenda kuisitiza hapa kwamba kwa kuonyesha upungufu wa walimu wa Kiswahili shuleni, hatuna maana kwamba masomo mengine yanajitosheleza kwa upande wa walimu, la hasha. Kusema kweli hata masomo ya sayansi na masomo mengine nayo pia yana upungufu mkubwa wa walimu. Isipokuwa mbinu zitumikazo kutatua matatizo ya upatikanaji wa walimu wa masomo ya sayansi na masomo mengine hutofautiana kwa kiasi kikubwa na zile za kupata walimu wa Kiswahili. Kupata walimu wa kufundisha masomo ya sayansi au masomo mengi-

HALI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI TANZANIA

ne, mbali na kutumia wahitimu wa kidato cha sita, wakuu wa shule hawachukui walimu kutoka shule za msingi. Pia walimu ambao hawakusoma masomo ya sayansi au masomo mengine katika vyuo vya ualimu/vyuo vikuu hawaombwi na wakuu wa shule kufundisha masomo hayo. Hali inapokuwa mbaya ya kukosa walimu hao, wakuu wa shule huajiri walimu wa muda wa masomo hayo kutoka shule za jirani na kuwalipa kutoka mfuko wa shule kama fedha zipo.

Tunachojaribu kuonyesha hapa ni kwamba suala la upungufu wa walimu wa Kiswahili shuleni halipewi uzito sawa ukilinganisha na walimu wa masomo mengine. Ni bahati mbaya sana imejengeka dhana kwamba mwalimu yeyote hata kama hakusomea Kiswahili chuoni anaweza kufundisha somo la Kiswahili. Hoja zinazotolewa kutetea msimamo huu ni kwamba kama mwalimu anazungumza Kiswahili vizuri atashindwaje kufundisha Kiswahili darasani? Tunaweza kusema kwamba watu wenye mawazo kama haya wanafikiri kwamba Kiswahili siyo somo muhimu na halihitaji utaalumu kulifundisha. Haya ni makosa kabisa. Kinyume na mawazo ya watu hao, Stubbs (1980) anakumbusha kwamba kufundisha lugha vizuri kunahitaji mtu aliyesomea mbinu za ufundishaji na siyo mwalimu yeyote. Mwalimu aliyesomea lugha anafahamu kwamba lugha za kundi moja huwa zina muundo na sarufi iliyo tofauti na lugha ambazo ziko katika kundi lingine. Kwa mfano, Kiswahili kina muundo na sarufi iliyo tofauti na ile ya lugha ya Kiingereza. Kwa mwalimu ambaye hakusomea kufundisha Kiswahili ni rahisi kwake kuchanganya miundo ya lugha hizi mbili katika kufundisha Kiswahili. Makosa kama haya yataepukwa ikiwa tu Kiswahili kitafundishwa na mwalimu aliyesomea kufundisha Kiswahili.

Kutothamini utaalumu wa walimu wa Kiswahili shuleni kunajionyesha katika mambo mengi, tutataja machache yafuatayo: Kwanza, wakati walimu wa masomo mengine huandaliwa semina za masomo yao na Wizara ya Elimu na Utamaduni na vyombo vingine vya elimu baada ya muda fulani kupita, hakuna semina yoyote iliyoandaliwa kwa ajili ya walimu wa somo la Kiswahili. Walimu waliohudhuria semina za Kiswahili za kanda, wote wamesema hawajawahi kuhudhuria semina yoyote ya Kiswahili tangu wamalize mafunzo yao ya ualimu vyuoni. Pili, wakati masomo mengine yanapewa kipaumbele na shule ya kununuliwa vifaa vya maabara, vitabu vya masomo hayo, somo la Kiswahili halipewi kipaumbele hicho. Kwa mujibu wa walimu wa Kiswahili, fedha zinazotolewa na shule kwa ajili ya kununua vitabu vya Kiswahili ni kidogo mno ukilinganisha na masomo mengine ukiacha masomo ya sayansi ambayo kimsingi huhitaji fedha nyingi kutokana na kununua vifaa mbalimbali vya maabara. Kwa mfano, shule nyingi hazina kamusi za kutosha za Kiswahili kwa ajili ya walimu, na wanafunzi, lakini shule nyingi zina kamusi za Kiingereza, au Kiingereza – Kiswahili. Pamoja na matatizo haya, yapo pia matatizo mengine ambayo tunafikiri yako nje ya uwezo wa mwalimu ambayo tutayajadili katika sehemu inayofuata.

3.3 Mchango wa Wizara ya Elimu na Utamaduni katika kukuza Kiswahili

Kwa sasa Wizara yenye dhamana ya kukuza, kuimarisha na kuendeleza Kiswahili nchini ni Wizara ya Elimu na Utamaduni (kwa kifupi, Wizara). Wizara hii yenye dhamana na Kiswahili

hutoa mipango ya kisera ambayo hutafsiriwa kwenye sera ya lugha, mihtasari ya masomo na kwenye asasi zinazokuza lugha ya Kiswahili. Kwa kuwa shule za msingi, shule za sekondari na vyuo vya ualimu ziko chini ya wizara hii, wizara haiwezi kukwepa tatizo la upungufu wa walimu shuleni. Kimsingi, wizara inatakiwa kupanga mikakati ya muda mfupi na muda mrefu ya jinsi ya kupata walimu wa kutosha sio tu walimu wa Kiswahili bali pia na walimu wa masomo mengine. Tatizo la ukosefu wa fedha ni la kisiasa zaidi kuliko kiutendaji. Kupanga ni kuchagua. Serikali ikipanga mambo yake vizuri kwa kufuata vipaumbele vya kitaifa, itafika wakati ambapo suala la upungufu wa walimu halitakuwa ni tatizo tena,

Suala la walimu wa Kiswahili kukosa kupata semina za Kiswahili kwa zaidi ya miaka 20 toka wahitimu mafunzo yao vyuoni, ni ushahidi tosha kwamba wizara haina mipango ya muda mrefu ya aina hii. Kama kweli wizara inayo mipango ya semina kwa walimu wake, inakuwaje kusifanyike semina ya Kiswahili hata moja katika kipindi chote cha zaidi ya miaka 20? Serikali inaweza kuwa kweli haina fedha; je, wataalamu wa wizara wanashindwa vipi kuandika mapendekezo ya utafiti ya kuombea fedha kwa wafadhili au mashirika mbalimbali ili walimu wa Kiswahili wapewe semina za kuwainua kitaaluma na katika mbinu zao za ufundishaji? Yapo mashirika ya nchi rafiki ambayo hutoa fedha kwa ajili ya semina za walimu wa masomo ya sayansi na masomo mengine, kwa nini wizara isifanye hivyo kwa somo la Kiswahili pia? Tunachotaribu kusema hapa ni kwamba hatuwezi kuinua kiwango cha elimu sekondari kama wizara haitoi semina za mara kwa mara kwa walimu wake. Ni jambo la kushangaza kuona mihtasari inafanyiwa marekebisho lakini watekelezaji wa mihtasari hiyo hawapewi semina za kuinua taaluma yao.

Tumesema pia kwamba mwenye dhamana ya kukuza, kuimarisha na kuendeleza Kiswahili hapa Tanzania ni Wizara ya Elimu na Utamaduni. Ni jambo la kusikitisha pia kuona kwamba wizara yenye dhamana na Kiswahili, lugha ya taifa, yenyewe inakuwa mstari wa mbele wa kukipiga vita Kiswahili kisitumike na wanafunzi wa sekondari wanapokuwa shuleni. Kwa mujibu wa walimu waliohudhuria semina za Kiswahili za kanda, wanadai kwamba shule zimepewa maagizo na wizara kwamba wanafunzi wote wanapokuwa shuleni wanatakiwa wazungumze Kiingereza wakati wote na mahali popote isipokuwa tu kwenye kipindi cha Kiswahili darasani. Ili kutekeleza agizo hili la wizara, kila shule inatakiwa iweke matangazo kwenye vibao yanayosomoka: *speak english*, yaani *zungumza kiingereza*. Wale wanafunzi wanaosikika kuzungumza Kiswahili darasani au nje ya darasa hupewa adhabu kwa kutotii agizo la kuzungumza Kiingereza. Adhabu hizi hutofautiana shule na shule.

Tunapenda kujua uhalali wa agizo la wizara la kumpa mwanafunzi adhabu kwa kuzungumza Kiswahili. Sisi tunafikiri kwamba agizo hilo halina uhalali wowote kisera, kielimu na hata kitaifa. Kusema kweli, agizo hilo siyo tu linaenda kinyume na haki za msingi za binadamu bali pia linakidhalilisha Kiswahili, lugha ya taifa, lugha rasmi inayotumika serikalini, bungeni, shuleni (shule za msingi), vyuoni (vyuo vya ualimu kwa wanaosomea ualimu daraja la IIIA), mahakamani (mahakama za mwanzo) n.k. Kwa nini wanafunzi wazuiwe kutumia lugha yao ya taifa shuleni wakiwa nje ya darasa? Kama lengo ni kutaka

HALI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI TANZANIA

kuwapa wanafunzi muda wa kutosha wa kuzungumza Kiingereza, kwa nini wasipewe uhuru wa kutumia lugha yoyote wanayoipenda? Hatuna uhakika kama njia hii ya kulazimisha wanafunzi kuzungumza Kiingereza inasaidia sana kuinua umilisi wao wa kuzungumza Kiingereza. Utafiti unatakiwa ufanywe ili kuthibitisha hili tunaloliuliza na ambalo hatuna uhakika nalo.

Tunapenda kutahadharisha hapa kwamba uamuzi huu wa kuwazuia wanafunzi kutumia Kiswahili siyo tu unakidhalilisha Kiswahili bali pia unakiua Kiingereza bila wizara yenyewe kujua. Ieleweke kwamba wanafunzi wanaopewa adhabu kwa sababu tu wamezungumza Kiswahili, kwanza hupatwa na hasira ya kupewa adhabu na pili huichukia na lugha yenyewe (Kiingereza) na matokeo yake baadhi ya wanafunzi hugeuka kuwa bubu. Lakini, hebu tujiulize swali, je, hakuna mbinu nyingine ambazo wizara au shule zinaweza kutumia kuhamasisha wanafunzi wapende kuzungumza Kiingereza bila kulazimika kuzuia wanafunzi wasitumie Kiswahili? Katika kutafuta mbinu zinazofaa, kwanza inafaa wizara au shule zenyewe zitafute na zielewe chanzo cha tatizo yaani, kwa nini wanafunzi wa sekondari wanashindwa kuandika na kuzungumza Kiingereza vizuri.

Tafiti zilizofanywa na wanataaluma mbalimbali (wakiwemo: Mlama & Matteredu 1978; Rubagumya 1996; Kiputiputi 2001) zinaonyesha kwamba tatizo linalosababisha wanafunzi wengi washindwe kuzungumza au kuandika Kiingereza vizuri katika masomo yao, siyo wanafunzi wenyewe bali ni mfumo mzima wa elimu ambao kimsingi unahitaji kufanyiwa tathmini ili uboreshwe. Kwa mfano, kuna haja ya kuboresha mafunzo ya ualimu vyuoni, mihitari iboreshwe, vitabu vya kiada/ziada pia vitazamwe upya, utungaji wa maswali ya mitihani pia nao uboreshwe, vifaa vya kufundishia vipatikane vya kutosha n.k. Kama tatizo ni mfumo wa utoaji elimu, basi tunashindwa kuelewa mantiki ya kulazimisha wanafunzi kuzungumza Kiingereza na kwa wale wanaoshindwa wapewe adhabu. Kwa nini wapewe adhabu kwa kosa ambalo si lao? Haya ni baadhi tu ya maswali ambayo wahusika wa Wizara wanapaswa kuyatolea majibu kwa manufaa ya umma kwa ujumla.

Mjadala huu kwa dhati yake hauna nia ya kukitetea Kiswahili na kukipuuza Kiingereza, la hasha. Kimsingi, tunataka kuona kwamba lugha zote mbili yaani, Kiswahili na Kiingereza zinatumiwa kikamilifu na wanafunzi wote shuleni. Hili linawezekana ikiwa mielekeo ya wanafunzi katika kuzitumia lugha hizo itakuwa chanya. Kuhusu mielekeo ya kutaka au kuto-taka kuzungumza Lugha ya Kigeni, Schooling (1990: 71) anaeleza kwamba:

- *Mtazamo chanya kuhusu Lugha ya Kigeni humchochea mtu kutaka kujifunza na kutumia lugha hiyo pindi nafasi ya kutumika inapatikana* (Tafsiri yetu).
- *Mtazamo hasi kuhusu Lugha ya Kigeni humfanya mtu achukie kila jitihada zinazofanywa za kutaka kuongeza matumizi ya lugha hiyo* (Tafsiri yetu)

Anachosema Schooling (1990) kinaweza kuwa na ukweli wa kiasi fulani katika mazingira ya Tanzania ya wanafunzi kutumia lugha ya Kiingereza katika shule za sekondari. Tunakuba-

liana na mawazo ya Schooling (1990) kwamba kwa mazingira ya Tanzania, wizara na shule za sekondari kwa pamoja zinatakiwa kujenga mazingira chanya kwa wanafunzi ili wao wenyewe wahamasike kutaka kujifunza Kiingereza kwa bidii na kukitumia kikamilifu na sio kulazimishwa kukitumia bila wao kupenda.

Zipo mbinu mbalimbali zinazoweza kutumiwa na walimu katika kuhamasisha utumiaji wa Kiingereza shuleni na hata nje ya mazingira ya shule. Kwanza, walimu wanaweza kuanzisha midahalo ya Kiingereza ya mara kwa mara miongoni mwa wanafunzi wenyewe na kuwashindanisha kividato yaani, kidato cha I na II, cha III na IV, na cha V na VI. Washindi wa kila kidato wapewe zawadi, siyo lazima iwe fedha taslimu, hata zawadi za madaftari, vitabu vya kusoma, ngao, vyeti, kuwapongeza washindi hadharani kwenye mabaraza ya wanafunzi wote, n.k. zaweza kutumika. Pili, shule inaweza kuanzisha mashindano ya kusoma vitabu mbalimbali vya Kiingereza na ikiwezekana wanafunzi washindanishwe ili waweze kuelezea kwa Kiingereza vitabu hivyo vinahusu nini. Tatu, wanafunzi bora wa kuzungumza Kiingereza mathalani watano kutoka kila darasa na kwa pamoja wapewe zawadi ya kutembelea mbuga za wanyama au sehemu yoyote inayovutia kielimu na waelekezwe kuwa wanaposafiri wajitahidi kuzungumza Kiingereza ili kujenga umilisi wao wa kutumia lugha ya Kiingereza. Hizi ni baadhi tu ya mbinu za uhamasishaji. Walimu wahimizwe kutumia mbinu nyingine mbalimbali wanazoona zinafaa kulingana na mazingira ya shule zao.

Tumejadili hoja hii ya wanafunzi kunyimwa haki ya kuzungumza Kiswahili shuleni kwa kirefu kwa sababu kuu mbili: Kwanza, mbali na hoja zilizotangulia kutolewa katika makala haya, hoja hii ina uzito mkubwa wa kuthibitisha madai yanayotolewa kwamba Kiswahili kinadhalilishwa shuleni kwa kutopewa haki yake ya kutumika kama lugha ya taifa kwa kisilingizio cha kulinda Kiingereza kisife. Pili, tulitaka pia tuthibitishe madai hayo kwa kutumia matokeo ya tafiti mbalimbali kwamba kuzuia wanafunzi kutumia lugha wanayoipenda hakufanyi wanafunzi hao wapende kuzungumza Kiingereza. Hoja na mifano mbalimbali tuliyotoa kuhusu suala hili, tunafikiri inatosha kwa kiasi kikubwa kuthibitisha madai kwamba kweli Kiswahili kinadhalilishwa katika shule za sekondari Tanzania.

4. Mapendekezo

Kwa kuzingatia uchanganuzi wa taarifa/data zilizopatikana kwa njia ya semina za Kiswahili za kanda zilizoendeshwa nchi nzima, tumegawa mapendekezo yetu katika makundi makuu matatu: Kwanza, yapo mapendekezo tunayofikiri yanaweza kutekelezwa na walimu wenyewe shuleni. Pili, yapo yale yanayohusu wakuza mitaala na tatu yapo mapendekezo ya kisera ambayo yanahusu wizara yenye dhamana ya kusimamia lugha kwa ujumla. Tuanze na pendekezo la kwanza.

4.1 Ufundishaji wa Kiswahili shuleni uboreshwe

Tumeona huko nyuma kwamba walimu wanalalamika kwamba hawana vitabu maalumu vya kuaminika vinavyoelezea nadharia za fasihi simulizi, fasihi andishi na uhakiki wa vitabu

HALI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI TANZANIA

mbalimbali. Kuhusu tatizo hili, tunapendekeza kwamba walimu wajenge tabia ya kupenda kusoma vitabu na majarida mbalimbali ili kujiongezea maarifa ya ziada. Kwa mfano, majarida yatolewayo na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ya *Kiswahili* na *Mulika* na lile la Idara ya Kiswahili la *Kioo cha Lugha* yamezungumzia mambo mengi ya kinadharia kuhusu lugha na fasihi ya Kiswahili kwa ujumla. Walimu wa shule moja pia wanashauriwa wapeane semina za Kiswahili za ndani miongoni mwao. Zile shule zilizo karibu zinaweza kuandaa semina za pamoja na kubadilishana utaalamu miongoni mwao au wanaweza kumwomba mtaalamu yeyote wa Kiswahili kutoka wilayani, mkoani (hususani wakaguzi wa Kiswahili wa kanda), mtaalamu kutoka TUKI au Idara ya Kiswahili ya chuo kikuu chochote ili aweze kutoa semina katika maeneo yanayowatatiza walimu.

Kama ilivyo kwa baadhi ya masomo mengine, walimu wa Kiswahili nao waunde vyama vyao vya Kiswahili kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa, kanda na taifa. Vyama hivi ni vya muhimu sana kwa sababu walimu wa somo moja wakikutana pamoja katika ngazi yoyote ile inakuwa rahisi kwa walimu hao kusaidiana kutatua matatizo yao ya ufundishaji bila hata ya ku-subiri semina zinazoandaliwa na wizara au Taasisi ya Elimu. Semina za ngazi ya juu zikifanyika zinakuwa zinaongezea utaalamu wa juu zaidi kwa faida ya walimu kuelewa maendeleo ya taaluma ya Kiswahili.

Tunashauri pia kwamba walimu watumie zana za kufundishia katika zile mada zinazohitaji kutumia zana ili kuinua kiwango cha taaluma cha wanafunzi. Si kweli kwamba somo la Kiswahili halihitaji zana za kufundishia. Wakuu wa shule nao wawe tayari kutoa fedha kwa ajili ya kununulia zana za kufundishia somo la Kiswahili kama vile wanavyotoa fedha kwa masomo mengine.

Muhtasari wa Somo la Kiswahili Uboreshwe

Muhtasari wa Kiswahili unaotumika sasa ulirekebisha kwa mara ya mwisho mwaka 1996. Inakaribia miaka kumi sasa muhtasari huu bado haujarekebisha. Kuna haja kwa Taasisi ya Elimu Tanzania kushirikiana na wadau wa Kiswahili hususani walimu wafundishao Kiswahili shuleni na vyuoni, wakaguzi wa somo la Kiswahili, Baraza la Mitihani, TUKI, Idara za Kiswahili za vyo vikiu ili kwa pamoja waweze kuupitia muhtasari huu wa Kiswahili (1996) na hatimaye watoe muhtasari mwingine ulioboreshwa na unaozingatia kukua kwa taaluma ya Kiswahili na maendeleo yake katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA). Katika mambo ya kuzingatia, muhtasari uangalie uwezekano wa kuongeza idadi ya vipindi vya Kiswahili kutoka vitatu (3) vya sasa kwa wiki hadi vinne (4) au vitano (5) kwa wiki. Ingefaa pia muhtasari uorodheshe vitabu vya Kiswahili vya kiada na ziada vinavyofaa kusomwa shuleni ili kuepuka upotoshaji wa taaluma ya Kiswahili. Utaratibu huu utaondoa kwa kiasi kikubwa tatizo la kuwepo kwa utitiri wa vitabu ambavyo kusema kweli baadhi ya hivyo vitabu utaalamu wake uko chini na hausaidii sana kukuza taaluma ya Kiswahili.

Tunapenda kuisisitiza hapa kwamba urekebishaji wa muhtasari ushirikishe wataalamu kutoka asasi za ukuzaji wa Kiswahili tangu hatua za mwanzo kabisa. Kuwashirikisha wataalamu

kwenye hatua za mwisho za kufanya warsha hakusaidii sana kuboresha muhtasari kwa sababu mara nyingi muda wa warsha huwa ni mfupi na kwa sababu hiyo sio mada zote hujadiliwa kwa ukamilifu wake. Sisi tunafikiri kwamba wataalamu wakishirikishwa mapema watapata muda wa kutosha wa kuwashirikisha wataalamu wenzao katika asasi zao ili kwa pamoja watoe maoni yao kabla ya mtaalamu aliyealikwa kwenda kwenye warsha ya kuupitia muhtasari unaohusika.

Wizara Isimamie Kikamilifu Maendelo ya Kiswahili

Kama tulivyosema huko nyuma, dhamana ya kukuza, kuimarisha na kuendeleza lugha ya Kiswahili imepewa Wizara ya Elimu na Utamaduni. Ni kutokana na kutambua umuhimu huu, tunapendekeza kwamba wizara iwe na mpango wa muda mfupi na muda mrefu wa kutoa mafunzo kwa walimu wengi iwezekanavyo ili kutatua tatizo la upungufu wa walimu wa Kiswahili shuleni. Pia katika mipango hiyo ya wizara, suala la kutoa semina za Kiswahili kwa walimu walio kazini lipewe kipaumbele. Pamoja na kuelewa kwamba lipo tatizo la upatikanaji wa fedha, tunapendekeza kwamba semina za walimu zifanyike angalau mara moja kila baada ya miaka mitatu. Semina za aina hii zinaweza kuendeshwa kila mwaka kwa kuanza na kanda mbili au tatu kupewa semina. Hii ina maana kwamba baada ya miaka mitatu kupita kila mwalimu katika kanda atakuwa amehudhuria semina ya Kiswahili. Utaratibu huu unazingatia ufinyu wa bajeti ya serikali. Kama hali ya fedha ni nzuri ingefaa walimu wapewe semina kila baada ya miaka mwili. Hii itasaidia kuinua kiwango cha elimu kwa ujumla.

Kuna haja kwa Wizara kuondoa agizo la kuwazuia wanafunzi kuzungumza Kiswahili shuleni. Agizo hili linaenda kinyume na haki za msingi za binadamu za mtu kutumia lugha anaoyipenda. Tunapendekeza kwamba wizara iwe inatoa maagizo shuleni ambayo yanasaidia kukuza, kuimarisha na kuendeleza lugha siyo tu Kiswahili bali pia na Kiingereza. Maagizo ya wizara yasionekane kupendelea lugha moja na kupuuza lugha nyingine. Kwa mfano, wizara itoe maagizo ya kuitaka kila shule iwe na maktaba yake na isisitize kwamba vitabu vya masomo yote vinunuliwe na viwekwe maktaba ili wanafunzi wengi wapate nafasi ya kwenda kuvisoma vitabu hivyo badala ya kuvifungia kwenye makabati ambako wanafunzi hushindwa kuvisoma kwa wakati wao wa nafasi.

5. Hitimisho

Katika makala haya tumejaribu kuchunguza hali ya Kiswahili katika shule za sekondari Tanzania. Katika uchunguzi wetu tuliweka mkazo wa kuangalia utumiaji wa Kiswahili ndani na nje ya darasa miongoni mwa wanafunzi ili kuona kama wana umilisi wa kutosha kuzungumza Kiswahili, lugha ya taifa. Lengo la uchunguzi huu lilikuwa ni kutaka kuthibitisha madai kwamba lugha ya taifa inadhalilishwa shuleni au la.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba Kiswahili hakipewi nafasi sawa ya kutumika shuleni kama ilivyo kwa Kiingereza. Tumeona pia kwamba idadi ya vipindi vya Kiswahili ni vichache (vipindi 3) ukilinganisha na vile vya Kiingereza (vipindi 6). Pili, tumeona pia kwa-

HALI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI TANZANIA

mba upungufu wa walimu wa somo la Kiswahili unapotokea, pengo hilo hujazwa na mwalimu wa somo lolote hata kama mwalimu huyo hakusomea Kiswahili. Mtindo unaotumika kwa walimu wa Kiswahili haufanyiki kwa masomo mengine. Upungufu wa walimu wa masomo mengine hujazwa na mwalimu mwenye sifa za kusomea za somo husika. Tatu, tumegundua kwamba walimu wa Kiswahili hawajawahi kufanyiwa semina yoyote ya Kiswahili tangu wahitimu mafunzo yao ya ualimu vyuoni. Walimu wa masomo mengine wameshawahi kufanyiwa semina za masomo yao ingawa siyo mara kwa mara. Nne, tumeona pia kwamba wizara imetoa agizo la kuzuia wanafunzi kuzungumza lugha ya Kiswahili ndani ya maeneo ya shule ili wanafunzi waweze kukuza umilisi wao wa kuzungumza Kiingereza.

Kwa kuzingatia agizo la wizara la kuzuia wanafunzi kuzungumza Kiswahili shuleni isipokuwa katika kipindi cha Kiswahili tu, na kwa kuzingatia hoja nyingine zilizotolewa hapo juu, utafiti huu unathibitisha kwamba hadhi ya Kiswahili shuleni imeshuka hasa ukizingatia kwamba adhabu hutolewa kwa wanafunzi wanaoonekana kuzungumza lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, tumetoa mapendekezo yanayohitaji kufanyiwa kazi na vyombo vya serikali ili kurudisha hadhi ya Kiswahili katika shule za sekondari Tanzania.

Marejeo

- Kihore, Yared M. 2001. Ufundishaji wa Sarufi Miundo ya Kiswahili katika Shule za Sekondari Tanzania. *Makala ya Kongamano la Kimataifa Kiswahili 2000*, imehaririwa na J. S. Mdee na H. J. M. Mwansoko. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Uk. 109-121.
- Kiputiputi, Omari M. 2001. Ufundishaji Sayansi kwa Kiswahili. *Makala ya Kongamano la Kimataifa Kiswahili 2000*, imehaririwa na J. S. Mdee na H. J. M. Mwansoko. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Uk. 350-373.
- Mdee, James S. 2001. Kamusi kama Rejeo muhimu la kujifunza Lugha: Mifano kutoka Kiswahili. *Makala ya Kongamano la Kimataifa Kiswahili 2000*, imehaririwa na J. S. Mdee na H. J. M. Mwansoko. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Uk. 243-265.
- Mlama, Penina M. & May N. B. Matteru 1978. *Haja ya Kutumia Kiswahili kufundishia katika Elimu ya juu*. Dar es Salaam: Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA).
- Msanjila, Yohana P. 1988. Uzoefu wa kutumia Kiswahili kama Lugha ya kufundishia katika Vyuo vya Ualimu Nchini Tanzania, *Journal of Linguistics and Language in Education* 3: 75-92. [Department of Foreign Languages and Linguistics. Dar es Salaam].
- Msanjila, Yohana P. 2005. Problems of Writing in Kiswahili: A Case Study of Kigurunyembe and Morogoro Secondary Schools in Tanzania, *Nordic Journal of African Studies* 14,1: 15-25.
- Nyerere, Julius K. 1968. *Education for Self Reliance*. Dar es Salaam: Government Printers.

YOHANA P. MSANJILA

- Qorro, Martha 1997. The Role and Place of Language in Education and Society: The Case of Kiswahili and English in Tanzania. *Papers in Education and Development* 18: 129-144.
- Rubagumya, Casmir M. 1996. *What Research Tells us about Language of Instruction in Tanzania*. Nairobi: IDRC.
- Rubagumya, Casmir M. 1999. Choosing the Language of Instruction in Post-Colonial Africa: Lessons from Tanzania. *Papers in Education and Development*.
- Schooling, Stephen J. 1990. *Language Maintenance in Melanesia: Sociolinguistics and Social Networks in New Caledonia*. Texas: Institute of Linguistics at the University of Texas.
- Stubbs, Michael 1980. *Language and Literacy: The Sociolinguistics of Reading and Writing*. London: Routledge and Kegan Paul.
- Wizara ya Elimu na Utamaduni 1997. *Sera ya Utamaduni*. Dar es Salaam.
- Wizara ya Elimu na Utamaduni 1996. *Muhtasari wa Kiswahili*. Dar es Salaam.